JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA KWANZA

26 JANUARI, 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 26 JANUARI, 2010

Wimbo wa Taifa Kuimbwa, Dua Kusomwa na
Kikao Kuanza Saa Tatu Asubuhi

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

1. MHESHIMIWA MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kwa kuwa, suala la uratibu wa Mambo ya Maafa si la Muungano ingawa maafa yenyewe hayana mpaka wala kiwango:-

Je, Serikali imejipanga vipi iwapo yatatokea maafa ya Baharini katikati ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

2. MHESHIMIWA DIANA MKUMBO CHILOLO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kwa kuwa, Jeshi la Polisi Wilaya ya Manyoni halina Ofisi ya kudumu na yenye hadhi ya Wilaya; na kwa kuwa, Ofisi ndogondogo zilizopo hazijakarabatiwa hadi sasa licha ya Serikali kuahidi kufanya hivyo; na kwa kuwa, Serikali ilishaamua kujenga kituo kipya cha Polisi cha Wilaya:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kituo hiki kipya cha Wilaya.

3. MHESHIMIWA DK. SAMSON FERDINAND MPANDA (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya

Ndani ya Nchi:- Kwa kuwa, kituo kidogo cha Polisi cha Somanga Kata ya Kinjumbi kilichojengwa na wananchi na wahisani mbalimbali kimekamilishwa kwa asilimia 75 (75%):-

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao ili kukamilisha kituo hicho.

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

4. MHESHIMIWA CASTOR RAPHAEL LIGALLAMA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Kwa kuwa, kuna baadhi ya wastaafu ambao walikuwa wanalipwa pensheni zao mpaka Januari 2008 bila matatizo; na ghafla malipo yakasitishwa baada ya mwezi Februari – 2008:-

(a) Je, ni nini kimetokea kwa wastaafu hao;

(b) Je, ni lini zoezi la kuhakiki wastaafu hao litafanyika Serikalini kama PPF ilivyofanya hivi karibuni kwa wastaafu wanaolipwa na mfuko huo;

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya wastaafu hao waliosimamishiwa malipo yao ya pensheni akiwemo na Hamisi M. Kasungura.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

5. MHESHIMIWA DKT. BINILITH SATANO MAHENGE (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kwa kuwa, Serikali kupitia **TANESCO** ilipanga na kutenga fedha Kwa ajili ya usambazaji wa umeme katika vijiji vya Mfumbi, Matamba, Ujuni na Mpangala Wilayani Makete kuanzia Januari 2009:-

(a) Je, utekelezaji wa miradi hiyo umefikia hatua gani hadi sasa;

(b) Je, ni miradi mingapi ya usambazaji umeme vijijini inatekelezwa na Wakala wa Umeme **(REA)** Wilayani Makete.

6. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kwa kuwa, Upungufu wa Nishati ya Umeme Nchini umekuwa ukiitatiza Serikali kwa muda mrefu sasa; na kwa kuwa, utafiti uliofanyika mwaka 2007 *(household survey)* unaonyesha kuwa wananchi waliounganishwa kwenye grid ya Taifa imeongezeka kwa asilimia 10 (2001) hadi asilimia 12 (2007), na katika ongezeko hilo maeneo yaliyo nje ya jiji la Dar es Salaam na ya vijijini yaliyounganishwa ni asilimia 2.5 (mwaka 2007) jambo linalofanya maeneo mengi kubaki katika hali mbaya sana:-

(a) Je, kuna ongezeko la asilimia ngapi kuanzia mwaka 2007 hadi 2010;

(b) Je, ni kwa kiasi gani ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa mwaka 2005 kuondoa tatizo la umeme imetekelezeka.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

7. MHESHIMIWA SHOKA KHAMISI JUMA (MICHEWENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Kwa kuwa, Elimu ya Juu ni muhimu kwa Taifa lolote kwa sababu inalenga kuwaandaa wataalamu mbalimbali kuja kukabidhiwa majukumu mazito katika jamii; na kwa kuwa, Serikali haitoi mikopo kwa wanafunzi wote walio na haki ya kujiunga na Vyuo Vikuu:-

(a) Je, serikali itakubaliana na mimi kwamba, umefika wakati wa kufanya juhudi zinazowezekana ili wanafunzi wote wanaoingia Vyuo Vikuu wapatiwe mikopo;

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kutowapatia mikopo wanafunzi wote kunawafanya baadhi ya wanafunzi kutokupata muda wa kutosha kushughulikia masomo na badala yake kutafuta fedha za ada na matumizi.

8. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Kwa kuwa, Serikali ilisema imeshahakiki madeni ya walimu na mchakato wa malipo hayo utaanza haraka iwezekanavyo:-

(a) Je, hadi sasa walimu wangapi wameshalipwa na wangapi hawajalipwa kwa mchanganuo wa kila mkoa Tanzania bara;

(b) Kwa kuwa; kumejitokeza malalamiko kwa baadhi ya walimu kulipwa fedha pungufu ya madai yao katika Mikoa mbalimbali kwa wale waliobahatika kulipwa; Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuwapatia

fedha zao zilizosalia haraka bila kikwazo chochote.

WIZARA YA MIUNDOMBINU:

9. MHESHIMIWA DKT. ABDALLAH OMAR KIGODA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu:- Kwa kuwa, Serikali katika barabara inazozijenga kwa kiwango cha lami ni pamoja na ile ya Korogwe – Handeni:-

(a) Je, ujenzi wa barabara hiyo umefikia wapi;

(b) Kwa kuwa; barabara hiyo ni muhimu kiusalama na kiuchumi katika kuunganisha Mikoa ya Magharibi, kati na Bandari ya Tanga; Je, ni lini barabara ya Handeni – Kibirashi – Kiteto – Kongwa itajengwa kwa kiwango cha lami.

10. MHESHIMIWA PHILEMON NDESAMBURO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu:- Kwa kuwa, Mji wa Moshi ndio mji wa Mlima Kilimanjaro ambao ndio unaoongoza kwa kuingiza pato kubwa la Utalii; Na kwa kuwa, **TANAPA/KINAPA** ina mpango maalum wa kukarabati njia zote zinazotumiwa na watalii kupanda Mlima Kilimanjaro:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kiwanja cha Ndege cha Moshi Mjini katika kukuza Utalii;

(b) Je, Serikali itakubali ombi la wakazi wa Moshi Mjini kuwa Kiwanja hicho

kihusishwe katika ukarabati kwani ni moja ya njia wanayotumia watalii.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

11. MHESHIMIWA DK. FESTUS BULUGU LIMBU (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Kwa kuwa, Serikali imeanzisha Bima ya Afya ya Jamii ambapo kila familia inatakiwa kutoa shilingi elfu kumi ili ipate matibabu na dawa bure kwa mwaka mzima kwenye Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya:-

(a) Je, Serikali ina taarifa kuwa mpango huo bado haujaeleweka kabisa kwa wananchi walio wengi;

(b) Je, Serikali inafanya mikakati gani ya kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusiana na mpango huo;

(c) Kwa kuwa, Zahanati na Vituo vingi vya Afya huwa havina dawa; Je, Serikali haioni kuwa, wananchi wanaumia kuchangia bima hiyo na kisha wanaandikiwa wanunue dawa kwenye maduka binafsi.

12. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Kwa kuwa, Sera ya Afya nchini inasema huduma za Afya ni bure kwa akina mama wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) na wazee wenye umri zaidi ya miaka sitini (60) wasiokuwa na uwezo; na kwa kuwa, zaidi ya asilimia themanini (80%) ya makundi hayo hawapati huduma hiyo bure:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza Watanzania fedha hizo zinazotengwa kila mwaka kwa

ajili ya makundi hayo zinakwenda kwenye mfuko gani na zinafanya kazi gani;

(b) Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikitoa maagizo mara kwa mara kwa Watendaji kutoa huduma hizo bure hospitalini; na kwa kuwa, sehemu kubwa ya maagizo hayo yatekelezwi; Je, ni Watendaji wangapi wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa kukiuka maagizo hayo ya Serikali na kusababisha adha kwa wananchi.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

13. MHESHIMIWA DR. ALI TARAB ALI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Kwa kuwa, kumekuwa na juhudi kubwa ya kupata mafuta kutoka kwenye mimea (Biofuel) na ardhi kubwa ya kilimo cha mazao ya chakula inatumika kwa ajili hiyo:-

(a) Je, umefanyika utafiti wa mafuta yatokanayo na Nazi kuona kama yanaweza kutumika kama nishati;

(b) Kama yanaweza kutumika hivyo, kwa nini minazi ambayo inaweza kulimwa na mazao mengine isilimwe kwa wingi zaidi kuliko Mibono na Miwa ambayo hairuhusu kulimwa pamoja na mazao mengine.

DODOMA **DKT. T.D. KASHILILAH**
26 JANUARI, 2010 **KATIBU WA BUNGE**